NISHATI
HABARI ZA NISHATI

News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 24 | Machi 1 - 31, 2021

# TATIZO LA UMEME SONGWE LAPATIWA MUAROBAINI

## Serikali imetenga takriban dola milioni 450 kujenga kituo cha kupoza umeme Songwe



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza kuhusu ufumbuzi wa tatizo la umeme mkoani Songwe wakati alipotembelea eneo la Mradi wa Nishati ya Jotoardhi lililopo katika eneo la Majimoto, Mkoani Songwe tarehe 31 Januari 2021 katika ziara ya kikazi mkoani humo.



## Byabato: Njooni muwekeze Singida Umeme upo wa kutosha

UK. 7



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

**Na Dorina G. Makaya - Songwe**

# TATIZO LA UMEME SONGWE LAPATIWA MUAROBAINI

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani amesema, Serikali imetenga takriban dola milioni 450 kwa ajili ya kujenga kituo cha kupoza umeme Songwe kitakachosambaza umeme Tunduma, Ikana, Laela hadi Kamsamba katika maeneo yote ambayo hayana miundo mbinu ya umeme.

Waziri Kalemani ameyasema hayo tarehe 31 Januari 2021 alipotembelea eneo la Majimoto lililoko wilaya ya Mbozi mkoani Songwe akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo.

Waziri Kalemani ameishukuru Serikali kwa kutenga fedha hizo zitakazowezesha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Songwe na kutatua tatizo la umeme mkoani Songwe.

Amesema, kuna takriban zaidi ya kilomita 2000 za mzunguko katika mkoa wa Songwe ambazo hazina kituo cha kupoza umeme na kueleza kuwa, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Songwe, utamaliza tatizo la umeme kutokuwa wa uhakika katika mkoa wa Songwe.

Dkt. Kalemani amesema, utaratibu wa ujenzi umeshaanza na kituo cha kupokea na kupoza umeme kitajengwa karibu na Tunduma na kusambaza umeme kuelekea Katavi na kuunganisha kwenda Kigoma ambapo itaunganisha hadi Geita - Nyakanazi.

''kuna grid inaitwa 'North West Grid' na kuwa, ukanda huu haukuwa na Grid ya Taifa na hivyo mkoa wa Songwe kuathirika kwa hilo. Lakini sasa kuna mpango madhubuti wa muarobaini wa kuondokana na kero hiyo na utekelezaji umeshaanza." Amesema Dr. Kalemani.

Waziri Kalemani ameongeza kuwa, ni kusudio la Wizara ya Nishati kuwa, ndani ya miezi 18, hali ya upatikanaji wa umeme mkoani Songwe itakuwa imerekebika na pia katika maeneo tajwa hapo juu.

Akizungumzia Kuhusu usambazaji wa umeme, Waziri Kalemani amefafanua kuwa, kukatika kwa umeme, kunasababishwa na Songwe kutokuwa na njia ya uhakika ya umeme. Amefafanua kuwa, hali ya umeme wa Mbeya na Songwe ni tofauti sana kwani Mbeya hawana shida ya umeme na kuwa kwa sasa mkoa wa Songwe



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akielekea kwenye eneo la Mradi wa Nishati ya Jotoardhi lililopo katika eneo la Majimoto, Mkoani Songwe tarehe 31 Januari 2021 katika ziara ya kikazi mkoani humo.

# TATIZO LA UMEME SONGWE LAPATIWA MUAROBAINI



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza kuhusu ufumbuzi wa tatizo la umeme mkoani Songwe wakati alipotembelea eneo la Mradi wa Nishati ya Jotoardhi lililopo katika eneo la Majimoto, Mkoani Songwe tarehe 31 Januari 2021 katika ziara ya kikazi mkoani humo.

unapata umeme kutoka katika kituo cha kupoza umeme cha Mwakibete, ambacho kina jumla ya MW 150.

Waziri Kalemani amebainisha kuwa, matumizi ya umeme ya mkoa wa Mbeya peke yake ni MW 75 na mkoa wa Songwe ni MW 15 kwa sasa, kwa hiyo umeme ulioko Mbeya, unatosha kutoa umeme kwa mikoa ya Mbeya na Songwe na kubakiza takribani MW 68.

Amesema, shida iliyopo ni njia ya kuusafirisha umeme huo ambayo ndiyo inajengwa na ni ndefu kwa kilomita za mzunguko 2010 na ndiyo maana kukosekana kwa kituo cha kupoza umeme kunasababisha tatizo la kukatika kwa umeme katika mkoa wa Songwe.

Amefafanua kuwa kutokana na njia ya umeme kuwa ndefu, kunahitilafu nyingi zinazotokea njiani na kusababisha kukatika kwa umeme lakini umeme unaozalishwa katika kituo cha Mwakibete unatosha kutoa umeme kwa Mikoa ya Mbeya na Songwe na kuwa na ziada.

Akizungumzia kuhusu usambazaji wa umeme kwenye vijiji vya mkoa wa Songwe, Dkt. Kalemani amekumbushia kuwa, wakati mpango wa kupeleka umeme vijijini unapangwa mwaka 2008, mkoa wa Songwe ulikuwa sehemu ya mkoa wa Mbeya na vijiji vingi vilivyopelekewa umeme, vilikuwa ni vijiji vilivyokuwa karibu na mkoa wa Mbeya.

Amesema, Mbeya ina vijiji takriban 502 lakini vijiji vilivyobakia kuunganishiwa na huduma ya umeme ni vijiji 91 tu na Mbeya ina vijiji vingi kuliko Songwe yenye vijiji vipatavyo zaidi ya 300 hadi 500. Lakini bado Songwe kuna vijiji 120 lakini vilikuwa pembeni sana na wakati huo kwenye mradi wa REA wa kupeleka umeme vijijini, Mbeya iliangaliwa kama mkoa wa Mbeya wakati huo Songwe haukuwa mkoa. Hivyo Songwe ilivyokuwa mkoa, ikaangukiwa na vijiji vichache vilivyokuwa kwenye mradi, lakini sasa muarobaini wake umepatikana.

Waziri Kalemani amemfahamisha Mkuu wa mkoa wa Songwe kuwa, Serikali imetoa jumla ya bilioni 851 kwa nchi nzima, kupeleka umeme katika vijiji vyote ambavyo bado havijaunganishiwa na huduma ya umeme.

Amesema, vijiji vyote vya Songwe vilivyobaki tayari viko kwa wakandarasi na Songwe imepatiwa wakandarasi wawili ili kuharakisha usambazaji wa umeme

# TATIZO LA UMEME SONGWE LAPATIWA MUAROBAINI

katika vijiji vya Songwe. Dkt. Kalemani amesema, utaratibu wa kuleta umeme kwenye vijiji hivyo, unaanza tarehe 02 Februari, 2021.

Waziri Kalemani ameweka bayana kuwa hapa Tanzania, kuna vijiji 12,268 lakini vijiji 10,109 tayari vina umeme ambapo ni vijiji 2059 tu ambavyo ni pamoja na maeneo ya vijiji vya Songwe na vitongoji ambavyo bado havijapelekewa huduma hiyo. Amesema vijiji vyote hivyo vitafikishiwa umeme ndani ya miezi 18 kuanzia tarehe 05 Februari, 2021.

Waziri Kalemani amebainisha kuwa Serikali imefanya kazi kubwa kwani wakati Serikali ilipoanza kupeleka umeme vijijini mwaka 2015 vijiji vilivyokuwa na umeme vilikuwa ni vijiji 2000 tu. Lakini leo vijiji vyenye umeme hapa nchini ni vijiji zaidi ya 10,000 vilivyounganishiwa na huduma ya umeme ndani ya miaka mitano.

Amesema kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vilivyobakia itakamilika ndani ya muda mfupi.

Waziri Kalemani ametoa wito kwa wakandarasi watakaopewa kazi ya kupeleka umeme vijijini, kuhakikisha wanafanya kazi hiyo ipasavyo na kukamilisha upelekaji wa huduma ya umeme kwenye vijiji na vitongoji ndani ya vijiji hivyo, inakamilika chini ya miezi 18.



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwa katika eneo la Majimoto la Mradi wa Nishati ya Jotoardhi Mkoani Songwe tarehe 31 Januari 2021 katika ziara ya kikazi mkoani humo kukagua utekelezaji wa Miradi ya umeme Mkoani Songwe na kuzungumza na wananchi kuhusu ufumbuzi wa tatizo la umeme mkoani humo. Upande wa Nyuma, kulia kwa Waziri Kalemani ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mha. Innocent Luoga na kushoto kwa Waziri Kalemani ni Meneja Mkuu wa kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC) Mhandisi Kato Kabaka (aliyeshika jiti).

Amesema baada ya hapo suala la kijiji katika nchi yetu kuwa hakina umeme litakuwa ni historia.

Aidha Waziri kalemani ameeleza kuwa, upelekaji wa umeme kuanzia sasa utakuwa shirikishi, ambapo Mkandarasi anapoingia kwenye maeneo ya wananchi, ataanza kuwaona viongozi wa maeneo husika ili wapewe maeneo ya vipaumbele kuhakikisha, maeneo muhimu kama taasisi za umma, yanapata umeme kwa haraka.

Dkt. Kalemani amewaomba viongozi wote wa taasisi zote, kuainisha maeneo yote ya kitaasisi ili wakandarasi wa REA wanapoanza kazi ya kuunganisha umeme, waanze na maeneo hayo kama maeneo ya vipaumbele.

"Unapopeleka umeme kwenye kituo cha afya, unahudumia zaidi ya wananchi 300 kwa mkupuo. kwa hivyo nitoe rai kwa wananchi, viongozi na wakandarasi wa mradi, kuzingatia maeneo ya kitaasisi kama kipaumbele." Amesema Dkt. Kalemani.

Katika ziara hiyo mkoani Songwe, Waziri Kalemani aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, pamoja na wataalam mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO.

# Dkt. Kalemani asema Corona haijaathiri upatikanaji wa mafuta nchini



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (katikati) na Kaimu Katibu Mkuu, Mhandisi Leonard Masanja(kulia) wakipata maelezo ya namna mafuta yanavyopimwa kutoka katika meli hadi kuwafikia walaji kupitia mita za kupimia mafuta(Flow Meter), wakati wa ziara ya waziri huyo ya kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, iliyofanyika Februari 07, 2021.

**Zuena Msuya Dar es Salaam,**

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani amewatoa hofu watanzania kwa kusema kuwa tishio la virusi vya ugonjwa wa corona halijaathiri upatikanaji wa mafuta nchini.

Aidha kuna ziada ya mafuta itakayotumika zaidi ya siku 30 na bado meli zinaendeleapakuwa mafuta bandarini.

Dkt. Kalemani alisema hayo Jijini Dar es Salaam, wakati wa ziara ya kutembelea bandari ili kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, kwakuwa nchi imeingia Uchumi wa Kati na miradi mingi mikubwa inaendelea kutekelezwa.

Alisema Tanzania imejipanga vizuri katika suala la upatikanaji wa mafuta, pia aliwatoa hofu watanzania kuwa serikali inaendelea vizuri katika sekta hiyo kwani mpaka sasa, hakuna kiwango cha mafuta kilichopungua tangu kutangazwa kwa uwepo wa ugonjwa huo duniani kote.

Alisema kwa sasa, nchi ina mafuta mengi na ya kutosha, pia ziada ya lita Milioni 209 kwa mafuta Petroli, mafuta ya Diseli lita Milioni 121, Mafuta ya Taa lita laki 6, na Mafuta Ndege lita Milioni 18, ambayo yatatosha kutumika kwa zaidi ya siku 30 zijazo na bado meli zinaendelea kupakuwa mafuta bandarini: Leo kuna meli inapakua Tani 38 za Mafuta.

Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuna mafuta ya kutosha siku zote ili miradi mikubwa ya kitaifa inayoendelea kutekelezwa kama vile ya SGR, Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere, Miundombinu ya Barabara, Maji na mingine



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kushoto), Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Erasto Simon (katikati) na Mhandisi Mkuu wa Vituo vya Upokeaji wa Mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam, Yona Malago( kulia)wakikagua eneo la kupakulia mafuta bandarini wakati wa ziara ya waziri huyo ya kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, iliyofanyika Februari 07, 2021.



Muonekano ya Sehemu ya mita za kupimia mafuta (Flow Meter) kutoka katika meli hadi katika mataki ya kuhifadhia mafuta, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, ya kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, iliyofanyika Februari 07, 2021.

# Dkt. Kalemani asema Corona haijaathiri upatikanaji wa mafuta nchini



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (wa pili kushoto), Kaimu Mkuregenzi Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Erasto Simon (kulia) wakiwa katika chumba maalum (Contolroom) kufuatilia upimaji wa mafuta yanayoingia nchini kutoka melini kwa kutumia teknolojia ya kisasa wakati wa ziara ya waziri huyo ya kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, iliyofanyika Februari 07, 2021.

mingi isikwame kwa kukosa mafuta kutokana na ugonjwa huo.

"Ninawahakikishia watanzania kwa niaba ya serikali kuwa mafuta yapo na yataendelea kuwepo, tumshukuru Rais wetu, Dkt. John Magufuli kwa msimamo wake thabiti kwani anatuwezesha kufanya kazi usiku na mchana, hivyo hatutaweza kuathirika kwa yanayosemwa, tumekaa na wadau pamoja na wataalamu wetu tumeweka mpango na mikakati ya kuhakikisha mafuta yanapatikana muda wote", alisema Dkt. Kalemani.

Kuhusu matumizi ya mafuta nchini, Dkt. Kalemani alisema kuwa matumizi yanaongezeka siku hadi siku, ambapo kwa sasa tunatumia Mafuta lita Milioni 5.7 ya Diseli, Petroli lita Milioni 4.6, Taa lita zaidi ya laki moja, na Ndege lita zaidi ya laki 6.



Mpira mweusi ukipakuwa mafuta Melini nakupita katika mita za kupimia mafuta (Flow Meter) hadi katika mataki ya kuhifadhia mafuta, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ya kujiridhirisha kama kuna mafuta ya kutosha kukidhi mahitaji yanayohitajika nchini, iliyofanyika Februari 07, 2021.

Aidha alisema kuwa, matumizi ya mafuta ya Taa yamepungua kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya umeme wa Gridi ya Taifa katika shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii vijijini.

Dkt. Kalemani alifafanua kuwa, Mwaka jana nchi ilikuwa na jumla ya mafuta ya ziada ya lita Milioni 325, mwaka huu kuna ziada ya lita Milioni 412, hivyo amewataka wataalamu wanaosimamia sekta hiyo kuhakikisha kiwango cha upatikanaji wa mafuta kinaongezeka zaidi.

Hata hivyo alisisitiza kuwa licha ya kuwepo kwa bandari, lazima kuendelea kupima na kuongeza uwezo wa bandari hizo nchini, ambapo kwa sasa imeongezeka bandari ya Tanga na Mtwara.

"Mpango mathubuti wa serikali ni kuangalia uwezekano wa kuongeza bandari kavu au maghala ya kuhifadhi mafuta katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Kagera zitakazotumika kuhifadhi mafuta ya takayosafirishwa nje ya nchi", alisisitiza Dkt. Kalemani.

Katika hatua nyingine, aliwataka wawekezaji kuja kufanya utafiti na kuwekeza katika sekta ya mafuta, kwa kuwa bei ya mafuta katika soko la Duniani inaendelea kuongezeka ikilinganishwa na miaka ya nyuma, na kueleza kuwa mwaka jana Pipa la mafuta ghafi lilikuwa Dola 50, ambapo kwa sasa ni Dola 57, Mafuta safi ilikuwa Dola 278, na sasa ni wastani wa Dola 446.

Katika ziara hiyo alitoa onyo kwa baadhi ya watanzania kuacha tabia ya kuhujumu miundombinu ya mafuta, ikitokea mtu amekamatwa kwa kosa hilo ahukumiwe kama wahujumu uchumi wengine kulingana na sheria za nchi: Pia Wataalamu pamoja na Timu ya Ulinzi na Usalama kuendelea kulinda na kusimamia miundombinu hiyo kwa maslahi mapana ya nchi na watanzania kwa ujumla.

# Byabato: Njooni muwekeze Singida Umeme upo wa kutosha

**Na Zuena Msuya**
**Singida,**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, amewataka wawekezaji Duniani kote kuja kuwekeza mkoani Singida kwakuwa kuna Umeme mwingi wakutosha na wa uhakika.

Alisema hayo alipokuwa akizungumza wakati wa Uzinduzi wa Mwongozo wa Uwekezaji mkoani Singida, uliofanyika Februari 22, 2021.



Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) na Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa Muongozo wa Uwekezaji Mkoani Singida, akimwakilisha Waziri Mkuu wa Tanzania, Kasim Majaliwa, Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Profesa. Kitila Mkumbo wakizungumza kabla ya Uzinduzi wa Muongozo wa Uwekezaji mkoani wa Singida, Februari 23, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato(kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Rehema Nchimbi (pili kushoto) wakibadilishana mawazo na uongozi wa Mkoa huo, baada ya kuwasili katika uzinduzi wa muongozo wa uwekezaji kwa mkoa wa Singida, Februari 23,2021.

Wakili Byabato alisema kuwa, kwa sasa mkoa huo unazalisha umeme wa Megawati 132, lakini mahitaji halisi ni Megawati 10.7 tu, hivyo kuna ziada ya Megawati 122.

Hata hivyo alisema kuwa mkoa huo pia, hivi karibuni unatarajia kukamilisha ufungaji wa mashine umba mpya itakayozalisha umeme wa Megawati 100, na hivyo kuufanya mkoa huo kuzalisha jumla ya Megawati 232, huku matumizi yakiendelea kuwa Megawati 10.7, na ziada itakuwa megawati 222.

"Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi hii, wenye Viwanda, Migodi, Wafanyabiasha mbalimbali na shughuli zote zinazohitaji umeme njooni Singida , tumieni hii fursa ya uwepo wa umeme mwingi, wakutosha na uhakika kuwekeza kwaku umeme ndiyo muhimili mkuu wa kuendesha shughuli zote za uwekezaji kwa kila Taifa Duniani", alisema Wakili Byabato.

Akizungumzia usambazaji wa Umeme

# Byabato: Njooni muwekeze Singida Umeme upo wa kutosha

vijijini, Wakili Byabato alisema kuwa, Vijiji 174 vimesalia kupata umeme kati ya vijiji 298 vya mkoa mzima wa Singida, ambapo aliahidi kuwa vijiji hivyo vyote vitawekewa umeme katika Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijiji (REA III) mzunguko wa pili unaoendelea kutekelezwa kuanzia Mwezi Februari mwaka huu.

Kwa upande wake Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo akimwakilisha, Waziri Mkuu wa Tanzania, Kasim Majaliwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Profesa. Kitila Mkumbo alisema kuwa wataalamu waliopewa dhamana ya kusimamia masuala ya uwekezaji wawe makini wakati wa mchakato wa majadiliano ya uwekezaji.

Aidha alisema kuwa ni muhimu wataalamu hao kuzielewa, kuzingatia na kuzijali na kuheshimu sheria za uwekezaji nchini kwa maslahi mapana ya nchi na wa Tanzania kwa jumla.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza wakati wa Uzinduzi wa Muongozo wa Uwekezaji kwa Mkoa wa Singida, Februari 23, 2021.

Prof. Mkumbo aliwasisitiza wataalamu hao kuzingatia uzalendo wa nchi na kuhakikisha kuwa uwekezaji husika unaleta tija na manufaa kwa taifa katika kuongeza uchumi badala ya uwekezaji huo kumnufaisha muwekezaji pekee.

Sambamba na hilo wataalam hao wametakiwa kuwapenda, kuwathamini na kuheshimiana na wawekezaji katika kila sekta ili kuendelea kuwavutia wawekezaji.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kulia) akitazama chupa ya Mvinyo katika mabanda ya maonyesho wakati wa Uzinduzi wa Muongozo wa Uwekezaji kwa Mkoa wa Singida, Februari 23, 2021.




Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (Tatu kulia) akipiga makofi baada ya kuzindulia kwa Kitabu cha Muongozo wa Uwekezaji Mkoani wa Singida, Februari 23, 2021.

# Dkt.Kalemani aagiza ujenzi wa kituo cha umeme Ifakara uanze ndani ya siku Kumi

**Na Teresia Mhagama, Morogoro**

Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Medard Kalemani, amemuagiza mkandarasi, kampuni ya AEE POWER EPC S.A.U kuanza ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme katika Mji wa Ifakara ndani ya siku Kumi, ili kuimarisha hali ya upatikanaji umeme katika Wilaya ya Kilombero pamoja na Ulanga mkoani Morogoro.

Dkt.Kalemani ametoa agizo hilo tarehe 23 Februari, 2021, wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro baada ya kufika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho na kubaini kuwa, kazi za ujenzi hazijaanza licha ya Mkataba kusainiwa mwezi Aprili mwaka jana.

"Haiwezekani mkataba usainiwe kutoka Aprili mwaka jana, lakini hata msingi hamjaweka, hapa kuna uwanja tu, mi nilitaka kuja kuona kazi zinazofanyika, si uwanja, hivyo naagiza Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini , Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wawe wameshafika katika eneo hili ifikapo tarehe 5 Mwezi ujao ili kuhakikisha ujenzi unaanza." Amesema Dkt. Kalemani

Waziri wa Nishati, amesema kuwa, Wilaya ya Kilombero na Ulanga zina changamoto ya



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (katikati), akisisitiza jambo wakati akizungumza na wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Epanko, Wilayani Ulanga, Mkoa wa Morogoro ambapo ameagiza kuwa migodi ya wachimbaji hao iunganishwe na umeme ndani ya Wiki Moja. Wa kwanza kulia ni Mbunge wa Ulanga, Mhe. Salim Almas



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (kulia) akizungumza na wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Epanko, Wilayani Ulanga, Mkoa wa Morogoro ambapo ameagiza kuwa migodi ya wachimbaji hao iunganishwe na umeme ndani ya Wiki Moja. Wa Tatu kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngollo Malenya.

# Dkt.Kalemani aagiza ujenzi wa kituo cha umeme Ifakara uanze ndani ya siku Kumi

kukatika kwa umeme mara kwa mara kwa sababu zinapata umeme kutoka vituo vya Kihansi na Kidatu ambavyo vipo mbali, na kupelekea Wilaya hizo kupata umeme hafifu.

Ameongeza kuwa, jumla ya shilingi Bilioni 23 zimetolewa na Serikali ya Tanzania pamoja na Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho hivyo hakuna sababu ya kuchelewesha ujenzi wa kituo husika, ambacho kinapaswa kukamilika mwezi Aprili mwaka 2022.

Aidha, akiwa katika Mji wa Ifakara, Dkt. Kalemani ametoa agizo kuwa, wananchi wanaoishi katika vitongoji, vijiji na mitaa iliyo pembezoni mwa miji na inafanana na vijiji, waunganishiwe umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu na si zaidi ya hapo.

Awali, Dkt. Kalemani alifanya ziara katika Wilaya ya Ulanga iliyokuwa na lengo la kukagua eneo la wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Epanko ili kuweza kuwapelekea nishati ya umeme itakayowawezesha kufanya uchimbaji wenye tija.

Akiwa wilayani humo. Dkt.Kalemani ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupeleka umeme kwenye migodi ya wachimbaji hao wadogo kuanzia wiki ijayo na kwamba kazi hiyo ifanyike kwa takriban kipindi cha mwezi mmoja.

Amesema kuwa gharama ya kupeleka umeme kwenye migodi hiyo ni takribani shilingi milioni 400 ambazo zipo na kwamba wananchi hao wataunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Vilevile, ametoa agizo kwa watendaji wa vijiji kote nchini kuhakikisha kuwa wanatenga fedha kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye Taasisi za Umma kwenye vijiji vyao ili kuwapa wananchi huduma bora ambapo gharama ya kuunganisha umeme kwenye Taasisi hizo ni shilingi 27,000 tu.



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (wa Tatu kutoka kulia) akikagua kazi ya ujenzi wa kituo kipya cha umeme katika Mji wa Ifakara, wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro. Pamoja naye ni Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa, (wa kwanza kushoto), Mbunge wa Kilombero, Mhe.Aboubakar Assenga (wa Pili kulia), pamoja na watendaji kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

# MENEJA TGDC APONGEZWA KWA UBUNIFU WA UENDELEZAJI NISHATI YA JOTOARDHI

**Na Augustino Kasale na Dorina Makaya – Songwe.**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard kalemani ameipongeza TGDC kwa ubunifu wa kutumia nishati ya jotoardhi si tu kwa kuzalisha umeme bali pia kwa matumizi mengine ya shughuli za kiuchumi.

Waziri Kalemani ametoa pongezi hizo alipoitembelea kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC katika eneo la Majimoto lililopo katika mkoa wa Songwe

Dkt. Kalemani amesema, wakati shughuli za uendelezaji wa nishati ya jotoardhi katika kuzalisha umeme zinaendelea tayari TGDC imefanya jitihada kwa kutengeneza fursa ya kutumia nishati ya jotoardhi kutotolesha vifaranga, kufugia samaki, shughuli za utalii, kukaushia mazao na shughuli nyingine.

"Niwapongeze sana TGDC kwa kutumia nishati ya jotoardhi kuzalisha umeme ukawa na manufaa mengine kwa jamii. Ni jambo zuri," amesema Waziri Kalemani.

Waziri Kalemani ameitaka TGDC kuwashirikisha wananchi ili waweze kunufaika na fursa ya uwepo wa



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akipatiwa maelezo ya mradi wa uendelezaji nishati ya jotoardhi katika eneo la Majimoto lililoko mkoani Songwe, anayetoa maelezo ni Meneja Mkuu TGDC Mhandisi Kato Kabaka (aliyeshika kijiti).



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani akigusa maji ya moto katika mojawapo wa chemchem ya majimoto ambacho ni chanzo cha nishati ya jotoardhi katika enelo la Majimoto mkoani Songwe, katikati ni Meneja Mkuu TGDC Mhandisi Kato Kabaka na Kaimu Mkurugenzi Maendeleo ya Biashara TGDC Mhandisi Shakiru Kajugus (kushoto).

nishati ya jotoardhi katika maeneo yao.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu TGDC, Mhandisi Kato Kabaka amemueleza Waziri Kalemani kuwa, kuwa licha ya TGDC kuendelea na uendelezaji wa nishati ya jotoardhi katika uzalishaji wa umeme, kuna teknolojia ambazo zimebuniwa na TGDC zikiwa na lengo la kuchangia katika shughuli za kiuchumi nchini.

"Mpaka sasa tumebuni teknolojia ya ututoleshaji vifaranga kwa kutumia nishati ya jotoardhi, kifaa cha kudhibiti joto la maji moto na kifaa cha kukusanya taarifa za utafiti wa nishati ya jotoardhi." Ameeleza Mhandisi Kabaka.

Akizungumzia kuhusu Mradi wa Umeme wa Jotoardhi 'Geo Thermo' Dkt. Kalemani amesema, hapa nchini tuna rasilimali, tuna uwezo na tuna vyanzo vingi vya umeme wa Jotoardhi na ndiyo maana Wizara ya Nishati imeanza kuvitembelea ili vifahamike vema.

Amesema, katika Mikoa ya Mbeya na Songwe pekee, tunayo miradi inayoweza kuzalisha zaidi ya MW 165 za Jotoardhi na kuna maeneo mengine kama vile Natron (Arusha), Luhoi (Pwani) na Kiejo Mbaka (Mbeya), Ngozi

# MENEJA TGDC APONGEZWA KWA UBUNIFU WA UENDELEZAJI NISHATI YA JOTOARDHI



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani akitazama mtambo uliobuniwa na TGDC wenye uwezo wa kukusanya taarifa za kisayansi za utafiti wa nishati ya jotoardhi na kuzituma kwa njia ya simu bila ya kuhitaji mtaalam kuwa eneo la utafiti.

(Mbeya) pamoja na Songwe (Songwe).

"Kwa ujumla hifadhi ya jotoardhi iliyopo hapa nchini inao uwezo wa kuzalisha zaidi ya MW 5000 katika miaka 10 ijayo tukijipanga vizuri." Amesema Dkt. Kalemani.

Amesema kwa kuanzia Wizara ya Nishati itaanza na MW 200 ambazo zitaanza kupatikana katika eneo la Majimoto lililopo katika mkoa wa Songwe ambapo kwa kuanzia litazalisha MW 5 hadi MW 38. na pia yapo maeneo mengine.

"Tunaanza na megawati 200 mojawapo ikiwa ni kutoka katika mradi huu wa jotoardhi Songwe, huku eneo hili peke yake likiwa na uwezo wa kuzalisha megawati 5 hadi 38." Amesema Dkt. Kalemani.

"Tanzania licha ya kuwa na jumla ya megawati 1602 kwa sasa, lakini bado hatuna hata megawati moja ya jotoardhi, ndio tunataka sasa tuharakishe." amesema Waziri Kalemani

Waziri Kalemani, amemtaka Meneja Mkuu wa kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), kuharakisha utengenezaji wa miundombinu itakayowezesha upatikanaji wa umeme unaotokana na Jotoardhi haraka na kumtaka kutumia miaka miwili kuanzia sasa kuanza kuzalisha umeme wa Jotoardhi usiopungua MW 200 kutoka kwenye vyanzo ili nchi ianze kunufaika na umeme wa nishati wa jotoardhi.

"Ningependa kuipongeza Serikali yetu kwa kutupatia shilingi bilioni 20 mwaka jana ili kuhakikisha miradi hii inatekelezwa," amesema Dkt. Kalemani.

Dkt. Kalemani ameongeza kuwa, hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 1.029, zimetumika katika uendelezaji wa shughuli za nishati ya jotoardhi katika Mradi wa Songwe.

Ameeleza kuwa, ili uweze kuzalisha umeme wa nishati ya jotoardhi kunahitajika nyuzi joto 100 hadi nyuzi joto 140, lakini joto linalopatikana kwa sasa ni nyuzi joto 70 mpaka 80 ambalo ndilo linalofaa kwa matumizi mengine ya nishati hiyo.

Akizungumza kuhusu utafiti wa Nishati ya jotoardhi, Mha. Kato Kabaka amemjulisha Waziri Kalemani, kuwa, shughuli za utafiti wa kina wa nishati wa jotoardhi katika miradi ya kipaumbele ya kuzalisha umeme zinaendelea na kwa sasa TGDC imefikia hatua ya uchorongaji visima vya jotoardhi ili kuhakiki kiwango cha hifadhi halisi ya jotoardhi iliyoko chini ya ardhi.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani akiwakabidhi wanakijiji wa eneo Majimoto (katikati) kuku waliototolewa na kukuzwa kutokana na nishati ya jotoardhi, kushoto ni Meneja Mkuu TGDC Mhandisi Kato Kabaka.

# Byabato: TANESCO malizeni kulipa fidia Simiyu kabla ya mwezi Machi mwaka huu

**Na Zuena Msuya, Simiyu**

Naibu Waziri wa Nishati,Wakili Stephen Byabato, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kukamilisha haraka zoezi la kuwalipa fidia wananchi waliobaki ambao wamepisha Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme kilichopo Kijiji cha Imalilo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, kabla ya mwezi Machi mwaka huu.

Wakili Byabato alitoa maagizo hayo, Februari 24, 2021 baaada ya kufanya ziara ya kutembelea eneo hilo linalotarajiwa kuanza kujengwa kituo hicho mwezi Julai mwaka huu, na kuzungumza na baadhi ya wananchi ambao bado hawajalipwa fidia kutokana na changamoto mbalimbali kujitokeza.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akitoa maelekezo kwa wasimamizi wa ujenzi wa kituo wakiwemo Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakati wa ziara ya kukagua eneo litakalojengwa Kituo cha Kupoza Umeme kilichopo Kijiji cha Imalilo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Februari 24, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati,Wakili Stephen Byabato (aliyenyoosha mkono) akiwaonyesha kitu wasimamizi wa ujenzi wa kituo wakiwemo Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakati wa ziara ya kukagua eneo litakalojengwa Kituo cha Kupoza Umeme kilichopo Kijiji cha Imalilo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Februari 24,2021.

Alitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni pamoja na kutofautiana kwa majina yaliyoandikwa katika vitambulisho vyao, nyaraka na hundi, zilizokuwa zikitumika kuwalipa fedha za fidia.

Aliweka wazi kuwa ni wananchi watano (5) tu kati ya Arobaini na Watano (45) waliopaswa kulipwa fidia bado hawajalipwa, Arobaini (40) tayari wamekwishalipwa na kuondoka kupisha mradi.

Kwa mantiki hiyo aliwaelekeza TANESCO kushirikiana na Idara na Taasisi husika ili kushughulikia na kumaliza changamoto hizo zinazokwamisha malipo ya wananchi hao, na kuhakikisha wanawalipa wote kabla ya mwezi machi mwaka huu, ambapo kunatarajiwa kuwekwa jiwe la msingi la kuanza ujenzi wa mradi huo.

Sambasamba na hilo, alitaka kuhamishwa kwa makaburi yaliyopo katika eneo hilo kwa kufuata utaratibu na sheria za nchi, kuzingatia haki ya kila alieyepisha mradi huo, kuepuka malalamiko kutoka kwa wananchi.

"TANESCO kamilisheni ulipaji wa fidia kwa waliobaki, hizi changamoto zao zinatatulika shirikianeni na mamlaka husika pitieni nyaraka na kufuata sheria zinazotakiwa muwalipe fedha zao hawa wananchi, ili waendelee na maisha yao na mradi uanze kujengwa hapa, hatutaki mradi huu

# Byabato: TANESCO malizeni kulipa fidia Simiyu kabla ya mwezi Machi mwaka huu



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kulia) akiangalia mchoro wa Ramani ya ujenzi wa Kituo Kupoza Umeme kilichopo Kijiji cha Imalilo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Februari 24, 202, wakati wa ziara ya kukagua eneo litakalojengwa Kituo hicho.

ulete malalamiko kwa wananchi tunataka haki itendeke kwa kila aliyepisha mradi huu na afurahie uwepo wake hapa, mapema mwezi Machi tutaweka jiwe la msingi, sitaki kusikia malalamiko siku hiyo", alisema Wakili Byabato.

Aidha katika ziara hiyo Wakili Byabato alitoa msisitizo kwa TANESCO, kuendelea kukata umeme kwa wadaiwa sugu ambao bado hawajalipa madeni ya Ankara zao na bado wanaendelea kutumia umeme.

Alisema ukataji wa umeme unawahusu wadaiwa wote bila kujali Taasisi, Mashirika ya Umma, Binafsi wala Dini.

Hata hivyo aliwasisitiza TANESCO kukata umeme kwa kuzingatia faida kwa maana kuwa mteja akilipa fedha kidogo atarejeshewa umeme kwa siku kadhaa, baadaye wakate tena hivyohivyo hadi pale atakapomaliza deni lake.

Vilevile wasikatae kupokea fedha ya mteja atakayoona anaweza kulipa kwa kipindi husika, wapokee wamuwashie baada siku kadhaa wakate tena.

Pia wawe na tabia ya kuwatembelea wadaiwa wao ili kuwakumbusha juu ya ulipaji wa madeni yao na kufanya ukaguzi ili kujiridhisha kama mteja aliyekatiwa umeme kwa muda mrefu anatumia nishati gani, hiyo itasaidia kubaini wateja wasiowaaminifu wanaoiba umeme.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kulia) akimshika bega mmoja wa wananchi wanaodai fidia wakati akizungumza naye kuhusu kumaliza changamoto inayomkabili mwananchi huyo ili alipwe malipo yake, alipofanya ziara ya kukagua Kituo Kupoza Umeme kilichopo Kijiji cha Imalilo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Februari 24, 2021.



Mmoja wa wanakijiji (katikati) ambaye bado hajalipwa fidia akimueleza jambo Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kulia) wakati wa ziara ya kukagua eneo litakalojengwa Kituo Kupoza Umeme kilichopo Kijiji cha Imalilo wilayani Bariadi mkoani Simiyu, Februari 24, 2021.

# Dkt. Kalemani aagiza, Mameneja wawili na Wahandisi wakuu watatu wa vituo vya umeme wasimamishwe

**Na Zuena Msuya**
**Dar es Salaam,**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ametaka Meneja wa Kituo cha Kupoza na Kusambaza umeme cha Kinyerezi I, Ubungo I pamoja na Mhandisi Mkuu wa Kinyerezi II, Kinyerezi I, na Ubungo I, wasimamishwe kazi na wachunguzwe kwa uzembe.

Dkt. Kalemani ametoa maagizo hayo, wakati wa ziara yake ya kukagua vituo hivyo na baadaye kuzungumza na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Februari 06, Jijini Dar es Salaam.

Aidha alitoa siku kumi na nne (14) kwa Bodi hiyo kuwafanyia uchunguzi mameneja na wahandisi wakuu hao na kumpatia majibu stahiki Waziri wa Nishati.

Dkt. Kalemani alisema kuwa, alifanya maamuzi hayo baada ya kubaini uzembe uliofanyika katika vituo hivyo, ikiwemo kutokuwepo kazini kwa watendaji hao na kutowajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao ya kazi.

"Haiwezekani Meneja na Mhandisi Mkuu wote wasiwepo katika vituo vyenu vya kazi bila sababu za msingi, mitambo yote inafanyiwa ukarabati kwa wakati mmoja! Hapana, hii haiwezekani ni uzembe wa hali ya juu lazima wachunguze na waondoe katika nafasi zao za kazi hawa watu wasije kutuletea matatizo", alisema Dkt. Kalemani.

Aidha aliiagiza Bodi ya TANESCO, kuhakikisha kuwa, mtaalamu wa kuunga kifaa cha kubusti umeme kilichopata hitilafu katika Kituo cha Kupoza umeme cha Kinyerenzi I, anapatikana na kufunga kifaa hicho ndani ya siku tatu (3) kuanzia leo na kituo hicho kizalishe umeme kama ilivyokuwa hapo awali.

Sambamba na hilo, aliwataka wataalamu wanaofanya ukarabati katika vituo hivyo kufanya kazi hiyo usiku na mchana ili kukamilisha matengenezo hayo haraka, ili kuruhusu vituo hivyo kuzalisha umeme wote unaotakiwa katika kituo husika.

Vilevile aliitaka Bodi hiyo kufanya ukaguzi katika vituo vya kupoza na kusambaza umeme



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) baada ya kufanya ziara ya kukagua vituo vya umeme vya Kinyerezi I, Kinyerezi II na Ubungo, Jijini Dar es Salaam, Februari 6,2021.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na mafundi wanaofanya ukarabati katika kituo cha umeme cha Kinyerezi wakati wa ziara ya kukagua kituo cha Kinyerezi I, Kinyerezi II na Ubungo na baadaye kungumza na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Jijini Dar es Salaam, Februari 6,2021.

# Dkt. Kalemani aagiza, Mameneja wawili na Wahandisi wakuu watatu wa vituo vya umeme wasimamishwe



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani, (kulia mbele) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka (kushoto) wakipita kukagua mitambo katika kituo cha umeme cha Kinyerezi, wakati wa ziara ya kukagua kituo cha Kinyerezi I, Kinyerezi II na Ubungo na baadaye kungumza na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Jijini Dar es Salaam, Februari 6, 2021.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na baadhi ya wahandisi wanaoendesha Kituo cha Umeme cha Ubungo, wakati wa ziara ya kukagua kituo cha umeme cha Kinyerezi I, Kinyerezi II na Ubungo, pia kungumza na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO),Jijini Dar es Salaam, Februari 6,2021.

ili kuona hali halisi ya uzalishaji wa umeme katika mitambo yote, na ndani ya kipindi cha miezi miwili (2) mitambo yote tisa (9) iwe inafanya kazi kwa ufanisi.

"Bodi muanze kufanya uchunguzi kwa wataalamu wanaosimamia mitambo ya umeme, na endapo mtabaini asiyemuaminifu na anayekwenda kinyume na maadili yake ya kazi, lazima achukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu mapema hata kabla ya wizara kuingilia kati", alisisitiza Dkt. Kalemani.

Katika hatua nyingine, aliwataka Mameneja TANESCO katika maeneo ya Chanika, Gongolamboto,Pugu na ukanda mzima wa maeneo hayo waeleze sababu ya kukatika kwa umeme katika maeneo hao mara kwa mara hali ya kuwa hakuna mgao na umeme upo mwingi wakutosha na ziada.

Alieleza wazi kuwa, endapo mameneja hao wameshindwa kutatua tatizo hilo ni dhahiri wameshindwa kufanya kazi, hivyo waondolewe katika nafasi hizo na wawekwe wale wenye uwezo wa kuwahudumia wananchi.

Akizungumzia suala la upatikanaji wa umeme nchini, Dkt. Kalemani alisema kuwa, hataki kusikia malalamiko ya wananchi kukosa umeme kwa sababu ya mitambo kuharibika, pia kuwaunganishia huduma ya umeme wale wote ambao wamekwisha lipia huduma hiyo kwa kuwa vifaa vipo vya kutosha, umeme upo mwingi na wakutosha.



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani, (kushoto) akizungumza na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania( TANESCO)(hawapo pichani) baada ya kufanya ziara ya kukagua Kituo cha Umeme cha Umeme vya Kinyerezi I, Kinyerezi II na Ubungo, Jijini Dar es Salaam, Februari 6,2021, kulia ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Leonard Masanja.

# Byabato : TANESCO toeni mafunzo kuboresha huduma kwa wateja

**Na Zuena Msuya, Manyara**

Naibu Waziri wa Nishati, Steven Byabato ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutoa mafunzo maalum ya mara kwa mara kwa vitengo vya kutoa huduma kwa wateja ili kuboresha utendaji kazi wa vitengo hivyo na kutoa huduma bora kwa wateja.

Byabato alisema hayo wakati wa mkutano wake na wafanyakazi wa Shirika hilo mkoani Manyara wenye wenye lengo la kufahamiana, kusikiliza changamoto zinazowakabili pamoja na kutoa maelekezo ya kuboresha utendaji kazi wa shirika hilo uliofanyika februari 17, 2021 mkoani humo.

Katika mkutano huo pamoja na mambo mengine, alisema kuwa vitengo vya kutoa huduma kwa wateja vimekuwa vikiongoza kwa kulalamikiwa na wateja kwa kutoa lugha isiyofaa na wakati mwingine hata



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati, Raphael Nombo, akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)mkoani Manyara kwa niaba ya Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, wakati wa mkutano wa Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, na wafanyakazi hao uliofanyika Februari 17, 2021 mkoani humo.



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Nchini( TANESCO) mkoani Manyara, wakati wa mkutano wake na wafanyakazi hao wenye wenye lengo la kufahamiana, kusikiliza changamoto zinazowakabili pamoja na kutoa maelekezo ya kuboresha utendaji kazi wa shirika hilo uliofanyika februari 17, 2021 mkoani humo.

# Byabato : TANESCO toeni mafunzo kuboresha huduma kwa wateja



Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Manyara, wakimsikiliza Naibu waziri wa Nishati, Stephen Byabato (hayupo pichani) wakati wa mkutano wake na wafanyakazi hao uliofanyika Februari 17, 2021 mkoani humo.

kutosikiliza wateja jambo linaloleta dosari TANESCO.

Aidha aliutaka uongozi wa TANESCO mkoani Manyara kujipanga na kutoka mafunzo kwa watumishi wake wa vitengo hivyo ya namna ya kuwa na lugha nzuri kwa wateja, kuwaelewesha wateja pale inapotekea changamoto, pindi wanawahudumia.

Aliweka wazi kuwa watuoa huduma kwa wateja katika Mkoa wa Manyara huo wamekuwa wakilalamikiwa sana na wateja jambo linaloleta dosari watumishi wote wa Mkoa huo

"Watumishi wa TANESCO msikubali watu wachache wakaharibu sifa ya shirika lenu ya kutoa huduma kwa wananchi, ninyi mmesambaa nchi nzima, hakikisheni mtoa mafunzo ya mara kwa mara katika vitengo hivi maana ndiyo kilio kikubwa kwa wateja, na mkiona mtu habadiliki basi mu,mumuonye na ikishindikana aondolewe kabisa", alisema Byabato.

Sambasamba na hilo aliwataka watoa numba za kulipia huduma ya umeme pamoja na watathmini ( Surveyor) kubadilika na kufanya kazi kwa kuzingatia weledi na taaluma zao kwa kuwa wamekuwa wakilalamikiwa sana kwa kuchelewa kutekeleza majukumu yao kwa wakati na hivyo kuleta



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Kata ya Bonga katika Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, wakati wa ziara yake mkoani humo iliyofanyika Februari 17, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (pili kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Baadhi ya wafanyakazi wa shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Manyara baada ya kumaliza mkutano wake na wafanyakazi hao uliofanyika mkoani humo, Februari 17,2021.

# Byabato : TANESCO toeni mafunzo kuboresha huduma kwa wateja

sifa mbaya kwa TANESCO.

Vilevile alitoa onyo kwa watumishi kuwa mahusiano ya kimapenzi sehemu za kazi kwa kuwa huharibu utendaji kazi, na kusabibisha watumishi hao kufanya kazi bila kuzingatia weledi na taaluma zao za kazi.

Alisema kuwa endapo watumishi wamependana katika eneo la kazi, wahalalishe mahusiano yao kwa kukufunga ndoa na baada ya hapo wanandoa hao kutenganishwa kutoka ofisi moja kwenda nyingine kwa maslahi ya ofisi husika na familia hiyo.

Kwa wale watakaobainika kuwa na mahusiano, kutoyaweka wazi kwa kuhalalisha, wakaharibu kazi kutokana na mahusiano yao, wachukuliwe hatua za kinidhmu.

" Hatutavumilia kuona kazi nzuri iliyofanywa kwa muda mrefu ikaharibiwa na watu wachache kwa kuwa tu ni wapenzi, unakuta mtu ana mahusiano na mwenzake hapo ofisini, wakija wateja atawahudumia tofauti ili mtu huyo aondoke, amlinde Mapenzi wake!hii hatutakubali mteja apate huduma mbaya, tukibaini tutakuondoa wewe kazini!", alisema Byabato.

Aliziagiza ofisi zote



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, (kulia) akikata utepe kuashiria kuwasha umeme katika moja ya nyumba ya wakazi wa mtaa wa Kandaka Kata ya Bonga, Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, wakati wa ziara yake mkoani humo iliyofanyika Februari 17, 2021. Katikati na kulia ni wenye nyumba iliyowashwa umeme Bwana na Bibi Kushque Nangai.



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (kulia) wakibadilishana mawazo na Meneja wa Shirika la Umeme Mkoa wa Manyara, Rehema Mashinji (kushoto) wakati wa Ziara ya Naibu Waziri huyo ya kuwasha umeme katika Kijiji cha Kandaka Kata ya Bonga katika Halimashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, iliyofanyika februari 17, 2021.

za TANESCO kote nchini, kuweka utaratibu wa kuwa na vikao vya mara kwa mara na watumishi wake katika kila idara na Vitengo, kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa hadi kanda ili kuweza kusikiliza changamoto zinazowakabili wafanyakazi wake na kuzitafutia ufumbuzi kwa wakati.

Alisema kuwa kwa kufanya hivyo kutawaweka wafanyakazi hao kufanya kazi kwa kasi zaidi, ubunifu mkubwa na usahihi pia kutaongeza ari ya kufanya kazi.

Aidha aliwataka watumishi wote kufanya kazi kwa kuheshimiana na kushirikiana kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu kwa kuwa watumishi wote wanategemeana katika utendaji kazi wao.

Katika mkutano huo aliwataka watumishi wa TANESCO, kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na kwa usahihi kama kauli mbiu ya Wizara ya Nishati inayoelekeza kwa wafanyakazi wote wa wizara hiyo na taasisi zilizochini yake.

Katika hatua nyingine, mara baada ya kumaliza mkutano na watumishi hao, akiwa njiani kuelekea Jijini Dodoma, Naibu Waziri huyo aliwasha umeme katika Mtaa wa Kandaka, Kata ya Bonga katika Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara.

# Byabato haridhishwi na kasi ya Ujenzi wa kituo cha kupoza Umeme Lemuguru



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (pili kulia) akipita kukagua Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo, Februari 17, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (kulia) akitoa maelekezo kwa wasimamizi na watekelezaji wa ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo, Februari 17, 2021.

**Na Zuena Msuya**
**Arusha,**

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato amekagua ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme wa 400kV cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha na kusema kuwa kasi ya ujenzi huo hairidhishi.

Byabato alisema hayo wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua kituo hicho iliyofanyika Februari 17, 2021 katika Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha akiwa njiani kuelekea mkoani Manyara.

Alisema kuwa kituo hicho kinatakiwa kukamilika mwezi wa Machi mwaka huu 2021, lakini baada ya kukagua na kuona hali halisi ya kasi ya Ujenzi inavyoendelea, haridhishwi na utekelezaji wa mradi huo.

Kufuatia hali hilo aliwataka wakandarasi wanaotekeleza Ujenzi huo pamoja na wasimamizi kufanya kazi usiku na mchana ili ili kuhakikisha kazi hiyo inakwenda haraka na kukamilika kwa wakati uliopngwa.

Hata hivyo Byabato alisisitiza kuwa, licha ya kuagiza kufanya kazi usiku na mchana, watekelezahi hao wafanya kazi kwa kasi, ubunifu na kwa usahihi kama kauli mbiu ya wizara inavyioelekeza na kusiepo kwa visingizio.

"Siridhiswi na kasi ya ujenzi unaoendelea hapa, kituo hiki kinatakiwa kumalizika haraka, wanachi



Baadhi ya nguzo zitakazobeba mitambo katika Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato alifanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho mkoani humo, Februari 17, 2021.



Wafanyakazi katika Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, wakimueleza jambo Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho, Februari 17, 2021.

# Byabato haridhishwi na kasi ya Ujenzi wa kituo cha kupoza Umeme Lemuguru



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato (pili kulia) akipita kuona hatua ya ujenzi wa jengo la maalum la kuendeshea mitambo (Control Room) wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, Februari 17, 2021.



Ujenzi wa nguzo zitakazobeba mitambo katika Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho, Februari 17, 2021.

wanataka umeme, kumbukeni kuna vijiji 19 vinategemea kupata umeme baada ya Kituo hiki kukamilika, ongezeni nguvu kazi, mfanye kazi usiku na mchana, na muifanye kwa usahihi, kasi na kwa ubunifu mkubwa", alisema Byabato.

Katika hatua nyingine alilitaka Shirika la Umeme nchini (TANESCO) kuharakisha kujenga barabara inayopita katika eneo la kituo hicho kwenda katika Kijiji jirani yenye urefu wa zaidi ya kilometa tatu (3), kwa kiwango cha changarawe kwa gharama nafuu kwa kuwa changarawe hiyo inapatikana maeneo hayo.

Aidha aliitaka TANESCO kushirikiana na uongozi wa kijiji hicho ili na wao wawe sehemu ya mradi huo, waone manufaa yake na kuharakisha ujenzi huo.

Naye Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi alimuomba Naibu Waziri hiyo kufuatilia malipo ya fidia kwa wananchi wachache waliobaki kulipwa baada kupisha mradi huo.

Aidha ameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Nishati kuendelea na kazi ya kusambaza Umeme katika vijijini mbalimbali nchini, na tayari mpango wa kuvifikia vitongoji vyote unaendelea.

Kituo cha kupoza umeme cha Lemuguru, kitatumika pia kusafirisha umeme 400kV hadi katika eneo la Isinya nchini Kenya, kitakuwa na uwezo wa kupoza umeme wa 222kV, na 35kV kwa ajili matumizi mengine.



Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, akikagua nguzo iliyokamilika kujengwa katika Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo, Februari 17, 2021.



Ujenzi wa jengo maalum la kuendesha mitambo ukiendelea, katika Kituo cha Kupoza Umeme wa Kilovolts 400 cha Lemuguru kilichopo wilayani Arumeru mkoani Arusha, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho, Februari 17, 2021.

# Bado Mwezi Mmoja na Nusu kuunganisha wateja waliolipia umeme-Dkt Kalemani

**Na Teresia Mhagama, Chato**

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani ametoa angalizo kwa watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwa, wamebakiwa na mwezi mmoja na nusu tu wa kuwaunganishia umeme wateja wote waliolipia umeme nchini.

Dkt.Kalemani ametoa angalizo hilo tarehe 17 Februari, 2021, wilayani Chato, Mkoa wa Geita



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwasha umeme katika moja ya nyumba zilizounganishiwa umeme kwenye Kitongoji cha Mwamatome, Kata ya Bwongera, wilayani Chato, Mkoa wa Geita.



Nyumba ya Ibada katika Kitongoji cha Mkombozi, Kata ya Muganza, wilayani Chato ambayo imeunganishiwa umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini.

wakati alipofanya ziara ya kukagua miundombinu ya umeme pamoja na kuwasha umeme katika Kitongoji cha Mwamatome na Mkombozi wilayani humo.

"Nilitoa muda wa miezi mitatu wa kuwaunganishia umeme wateja wote waliolipia nchi nzima, mwezi mmoja na nusu tayari mmeshautumia, sasa mmebakiwa na mwezi mmoja na nusu tu, hivyo waunganishieni umeme wateja wote waliolipia." Amesema Dkt.Kalemani

# Bado Mwezi Mmoja na Nusu kuunganisha wateja waliolipia umeme-Dkt Kalemani

Kuhusu wateja ambao wanasubiri kupimiwa maeneo yao ili kuunganishwa umeme, amesema kuwa, alishatoa agizo kwa wapimaji wa maeneo wa TANESCO, (surveyors) kununuliwa pikipiki ili kukamilisha upimaji wa maeneo na kwamba ifikapo mwisho wa mwezi wa Pili wawe wameshanunuliwa pikipiki hizo.

Vilevile, kuhusu maendeleo ya kazi ya uunganishaji umeme vijijini nchini, amesema kuwa, hadi sasa jumla ya vijiji 10,263 vimeshaunganishiwa umeme na vijiji vilivyobaki ambavyo vinaendelea kuunganishiwa umeme ni 2,005.



Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), wakati akizungumza na wananchi wa Kitongoji wa Mwamatome, wilayani Chato, Mkoa wa Geita.



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwasha umeme katika Kitongoji cha Mkombozi, Kata ya Muganza, wilayani Chato, Mkoa wa Geita. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho.

Akizungumza na wananchi wa vitongoji hivyo, Dkt.Medard Kalemani amesisitiza kuhusu matumizi ya kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) ambacho kinawawezesha wananchi kupata umeme bila kuingia gharama za kufunga mfumo wa nyaya katika nyumba.

Pia, amesisitiza kuwa, bei ya kuunganisha umeme vijijini ni shilingi 27,000 tu na kwamba kila nyumba inastahili kupata umeme.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho, amesema kuwa, kuunganishwa kwa umeme kwenye vitongoji vya Mwamatome na Mkombozi, wilayani humo kutawawezesha wananchi kuweza kufanya biashara mbalimbali na kuanzisha viwanda vidogovidogo.

# Naibu Waziri Byabato, apongeza ujenzi wa kituo cha umeme wa 400kV Singida

## Apiga Marufuku mapenzi sehemu za kazi



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (katikati) akiwaeleza jambo wasimamizi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Singida, wakati wa ziara yake ya kukagua kituo hicho, iliyofanyika Februari 22, 2021, mkoani humo.

**Na Zuena Msuya Singida,**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amepongeza kasi ya ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme wa 400kV cha Singida ambacho ujenzi wake umefikia asilimia 94 na kinatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni mwaka huu.

Wakili Byabato alitoa pongezi hizo wakati wa ziara yake mkoani Singida, Februari 22, 2021, ya kukagua Kituo hicho na kuzungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani humo, kwa lengo la kufahamiana, kusikiliza changamoto zinazowakabili pamoja na kutoa maelekezo ya kuboresha utendaji kazi wa shirika hilo.

Aidha alisema kuwa kazi kubwa zote zinazohusufu mfumo wa umeme katika kituo hicho zimekamilika, na kinachoendelea sasa ni kukamilisha kazi ndogondogo ikiwemo ukarabati wa mazingira katika eneo husika.


“Nawapongeza sana wakandarasi wanaotekeleza ujenzi wa kituo hichi, wamejenga kwa kasi inayotakiwa, na inavyoonekana hapa wanaweza kukabidhi mradi huu kabla ya muda uliopangwa, hata watanzania wakiona kazi hii watafurahi na kuona fedha zao zinafanya kazi ipasavyo ya kuwaletea maendeleo kwa haraka zaidi kupitia Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais wetu Dkt. John Magufuli”, alisema Wakili Byabato.

Nawasisitiza wawekezaji wa ndani na nje ya Tanzania, kuja kuwekeza mkoani Singida kwa kuwa mkoa huu una umeme mwingi zaidi ya mahitaji husika, wauhakika, wakutosha na ziada.

Aidha alisema kuwa mazingira ya uwekezaji ni salama na rafiki wakati wote kwa wenye viwanda, migodi na shughuli zote zinatohitaji umeme.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo, alipiga marufuku mahusiano ya kimapenzi sehemu za kazi kwa wafanyakazi na watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kuwa yanaharibu na kuzorotesha utendaji kazi.

Alisema kuwa kujihusisha na mapenzi sehemu za kazi kunasababisha watumishi na wafanyakazi hao kufanya kazi pasipo kuzingatia



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akionyeshwa namna ambavyo Kituo cha Kupoza Umeme cha Singida kinavyofanya kazi kupitia teknolojia ya kisasa, wakati wa ziara yake ya kukagua kituo hicho, iliyofanyika Februari 22, 2021, mkoani humo.

# Naibu Waziri Byabato, apongeza ujenzi wa kituo cha umeme wa 400kV Singida



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akionyeshwa namna ambavyo umeme wa 400kV, utakavyokuwa unaingia katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Singida wakati ziara yake ya kukagua kituo hicho, iliyofanyika Februri 22, 202, mkoani humo.

sheria na maadili pamoja na weledi katika taaluma zao, pia ni kosa kisheria.

Alieleza wazi kuwa, wenye mahusiano sehemu za kazi wayahalalishe kwa kufunga ndoa, ili mmoja kati yao ahamishie ofisi nyingine kiutendaji kwa faida ya taasisi husika na familia kwa jumla.

"Marufuku mahusiano ya mapenzi kazini, ukiwa na mpenzi ofisini huduma zinazotorota, natoa mfano kiongozi akiwa na mahusiano msaidizi wake, lazima kazi zitalegalega na nyingine kutofanyika kabisa, mteja ama mtumishi mwingine atataka kuona na kiongozi husika au kufikisha ujumbe, lakini mpeleka ujumbe anaweza asiufikishe kwakuwa tu hataki mpenziwe asumbuliwe ama ashikwe na wivu, msikubali kazi kuharibiwa kwa starehe za wengine", alisisitiza Wakili Byabato.

Wakili Byabato alifafanua kuwa, kwa wale watakaokuwa na mapenzi ya siri sehemu za kazi, wakibainika watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za kazi nchi.

Halikadhalika alipiga marufuku kwa watumishi hao kujihusisha na vitendo vya rushwa na kueleza kuwa baadhi ya watumishi wamekuwa wakiweka mazingira ya kupewa rushwa ili kutekeleza majukumu yao.

Alitaja miongoni mwa mazingira wanayotengeza watumishi hao ili wapate rushwa, kuwa ni pamoja na kutotimiza wajibu wao kwa wakati na kuchelewa kutoa huduma kwa wateja pamoja na kufanya uzembe.

Vilevile alitaka kila ofisi ya TANESCO nchini kutenga fungu maalum la fedha kwa ajili ya kuwapatia madereva pamoja na wahudumu wa ofisi zitakazowasaidia watu hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Alisema kuwa watumishi hao wamekuwa wakitumia fedha zao binafsi kufanya shughuli mbalimbali, akitolea mfano kwa madereva kuwa wamekuwa wakiziba pancha, kuosha magari nk.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (katikati) akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Singida,(hawapo pichani), kulia ni Kaimu Meneja Mwandamizi,Kanda Kati, Mhandisi Cecilia Msangi, kushoto ni Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Mbadala wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Edson Ngabo, wakati wa ziara ya Naibu Waziri huo mkoani humo, Februari 22,2021.

# TANESCO fanyeni mikutano ya mara kwa mara na wafanyakazi wenu



Naibu Waziri Wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Simiyu, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 25, 2021.

**Na Zuena Msuya Simiyu**

Naibu Waziri Wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kufanya vikao vya mara kwa mara na wafanyakazi wa shirika hilo kwa kila Kitengo na Idara husika ili kusikiliza changamoto zinazowakabili watumishi hao.

Wakili Byabato alisema hayo, wakati akizungumza na wafanyakazi wa shirika hilo mkoani Simiyu Februari 25, 2021, wakati wa ziara yake mkoani humo.

Alisema vikao hivyo vihusishe wafanyakazi wote bila kujali viwango vya elimu na ngazi za madaraja walizonazo, ili kila mtumishi aweze kueleza yanayomsibu sehemu za kazi pamoja na kueleza namna bora ya kuboresha utendaji kazi wao.

Aliwaeleza kwamba vikao hivyo ndivyo vinavyowafanya wafanyakazi kujiona wao ni sehemu ya familia ya shirika kwa kuwa wanapata muda wa kukaa pamoja na kuzungumza na viongozi wao.

Aidha alitaka watumishi hao kupewa nafasi ya kutoa maoni au mapendekezo yao ya nini kifanyike ili kuboresha utendaji kazi wao pamoja na shirika kwa jumla na maoni hayo yasikilizwe na kufanyiwa kazi.

"Mfanyakazi hutumia muda mwingi wa maisha yake sehemu ya kazi, eneo hili ni muhimu sana kwa kuwa wote hujiona ni familia moja licha ya kila mmoja kutekeleza majukumu yake, hivyo ni muhimu viongozi wa eneo husika kuweka utaratibu kuwa na vikao vya pamoja ili waweze kueleza changamoto zao, na zifanyiwe kazi kwa wakati sahihi, hii inaongeza morali ya kufanya kazi muda wote kwa kasi, ubunifu na usahihi, na katika vikao hivyo mara nyingi hupatikana mawazo chanya ya kujenga na kuimarisha zaidi ubora wa shirika", alisema Wakili Byabato.

Katika hatua nyingine aliwaonya watumishi hao kufika kazini wakiwa wamelewa ama kunya pombe muda wa kazi, na atakayebainika kuwa na tabia hiyo achukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za kazi.

# TANESCO fanyeni mikutano ya mara kwa mara na wafanyakazi wenu





Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Simiyu, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza nao wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 25, 2021.

Hata hivyo alipongeza wafanyakazi wa shirika hilo mkoani humo kuwa wamekuwa wakifanya kazi zao kwa umakini na kutoa huduma nzuri kwa wateja licha ya changamoto mbalimbali zinazowakabili za kukatika umeme mara kwa mara mkoani humo.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (katikati walioketi) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Simiyu, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 25, 2021.

Aidha aliwaeleza kuwa waendelee kuwa wavumilivu kwakuwa muda si mrefu changamoto hiyo itatuliwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Imalilo.

Kituo hicho kitakuwa na uwezo kuzalisha umeme wa Megawati 90 itakayokuwa ikitumika katika mkoa huo na mikoa jirani, mahitaji ya umeme kwa Simiyu kwa sasa ni Megawati 10 tu.

Mkoa wa Simiyu unapokea umeme kutoka mkoani shinyanga na hivyo kuufanya umeme huo kuwa na nguvu ndogo kuhimili matumizi halisi.

# Naibu waziri wa Nishati asisitiza kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na usahihi



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati wa ziara yake mkoani Mara, Februari 26, 2021.





Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akishiriki dua na sala kabla ya kuanza kwa mkutano wake na wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) alipofanya ziara mkoani Mara, Februari 26, 2021.

**Na zuena msuya mara**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, ametaka wafanyakazi wa shirika la umeme tanzania ( TANESCO) kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na usahihi kwa maslahi mapana ya nchi na taifa kwa jumla.

Wakili Byabato alisema hayo wakati wa ziara yake mkoani Mara, Februari 26,2021, ambapo alizungumza na wafanyakazi wa (TANESCO) pamoja na kutembelea Kituo cha Kupoza Umeme cha mkoa huo kinachozalisha Megawati 24, matumizi halisi kwa sasa yakiwa ni megawati kumi nukta saba (10.7).

Alisema kuwa kwa kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na usahihi kutawezesha shirika hilo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuwahudumia watanzania wote kwa wakati sahihi.

“Wafanyakazi wa TANESCO wanadhamana kubwa ya kuhakikisha kuwa umeme unasambaa Tanzania nzima kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, ni wakati sahihi kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na usahihi ili kutimiza azma ya serikali ya kufikisha umeme kwa watanzania wote na kukuza uchumi wa viwanda”, alisema Wakili Byabato.

# Naibu waziri wa Nishati asisitiza kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na usahihi



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akiteta jambo na kaimu meneja wa shirika la umeme tanzania ( TANESCO) Mhandisi Hamis Kadoma( kushoto) wakati wa mkutano wake wafanyakazi wa Shirika hilo mkoani humo alipofanya ziara Februari 26, 2021.



Baadhi ya Wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), mkoani Mara wakimsikiliza, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, (hayupo pichani) wakati wa mkutano wake na wafanyakazi hao alipofanya ziara mkoani humo, Februari 26, 2021.

Akizungumzia kituo cha kupoza umeme cha mkoa wa Mara, alisema kuwa kituo hicho kilizinduliwa mwaka 1989 na kinapokea umeme kutoka katika maeneo manne (Fider) ambayo ni katikati ya mji wenye wa Mara, Butiama, Tarime na Majita.

Aidha alisema kuwa, hivi karibuni serikali inatarajia kutanua kituo hicho ili kongeza uwezo wake wa kuzalisha umeme.

Vilevile aliwataka wawekezaji kuwekeza katika mkoa huo kwa kuwa kuna umeme mwingi na wa kutosha.

Katika hatua nyingine aliwataka watanzania kulinda miundombinu ya umeme iliyopita na kusambazwa katika maeno yao.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akisani kitabu cha wageni alipotembelea Kituo cha Kupoza Umeme cha Mkoa wa Mara, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 26, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato(kulia), akitoa maelekezo kwa watendaji katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Mkoa wa Mara, alipotembelea kituo hicho, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 26, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato(katikati), akipata maelezo jinsi Kituo cha Kupoza Umeme cha Mkoa wa Mara kinavyofanya kazi, alipotembelea kituo hicho, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 26, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato(kushoto), akionyesha katika mitambo ya kupoza umeme katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Mkoa wa Mara, alipotembelea kituo hicho, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 26, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto), akionyeshwa kitu katika mitambo ya kupoza umeme katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Mkoa wa Mara, alipotembelea kituo hicho, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 26, 2021.



Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Singida wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, (hayupo pichani), wakati akizungumza na wafanyakazi hao wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 22, 2021.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, (katikati mbele suti ya blue) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Singida, wakati wa ziara yake mkoani humo, Februari 22, 2021.



Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mha. Innocent Luoga, akifuatilia kwa umakini maelezo ya Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, (Hayumo Pichani) alipokuwa akizungumza kuhusu hali ya upatikanaji wa umeme Mkoani Njombe mara alipotembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe tarehe 30 Januari, 2021 kufuatia ziara yake ya kikazi mkoani humo.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Njombe (Hayumo pichani) pamoja na watengaji wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, kufuatia maelezo ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe Bi. Katarina Tengia Revocati kuhusu hali ya upatikanaji wa umeme Mkoani Njombe, mara alipotembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe tarehe 30 Januari, 2021 kufuatia ziara yake ya kikazi mkoani humo.

Katika ziara hiyo Waziri Kalemani aliambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme Mha. Innocent Luoga pamoja na timu ya Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO.

Katibu Tawala Bi. Katarina Revocati, amesifia kuhusu hali ya upatikanaji wa umeme Mkoani Njombe na kueleza kuwa, taarifa za ukataji wa umeme pale inapotokea dharula zinatolewa kwa wakati.

Waziri Kalemani ametoa muda wa siku 90 kwa Mkandarasi wa Mkoa wa Njombe Kukamilisha Mradi wa kupeleka umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza kuhusu ukamilishaji wa Mradi wa kupeleka umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza kwa Mkoa wa Njombe, katika ofisi ya CCM Wilaya ya Makete tarehe 30 Januari, 2021. Kulia kwa Waziri Kalemani, ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe Bw. Jassel Job Mwamwala.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili kwenye ofisi za CCM Wilaya ya Makete, tarehe 30 Januari, 2021. Kulia kwa Waziri Kalemani ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe Bw. Jassel Job Mwamwala na anayefuatia ni Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Marwa Mwita Ribirya.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza kuhusu ukamilishaji wa Mradi wa kupeleka umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza kwa mkoa wa Njombe katika Ofisi ya CCM Wilaya ya Makete, tarehe 30 Januari, 2021. Kulia kwa Waziri Kalemani ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe Bw. Jassel Job Mwamwala.



Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mha. Innocent Luoga ( wa Kwanza Kulia) akifuatilia kwa umakini maelezo ya Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Hayumo Pichani) alipokuwa akizungumza kuhusu ukamilishaji wa Mradi wa kupeleka umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza kwa mkoa wa Njombe katika Ofisi ya CCM Wilaya ya Makete tarehe 30 Januari, 2021 akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Njombe. Kushoto kwa Kamishna Msaidizi wa Umeme Mha. Luoga ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Uzalishaji wa Umeme TANESCO, Mha. Pakaya Mtamakaya.



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Makete tarehe 30 Januari, 2021 wakati alipotembelea eneo la Mradi wa kufua umeme wa Rukamali utakaozalisha 222 MW. Kulia kwa Waziri Kalemani ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mha. Innocent Luoga na kushoto kwa Waziri Kalemani ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe Bw. Jassel Job Mwamwala.

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI




***Fika Ofisi ya Mawasiliano,***
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*